

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE

Kumb. Na.HWK/S.1/22/VOL.I/133

01/08/2024

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe anatangaza nafasi (3) za kazi. Tangazo hili limetokana na **kibali cha ajira kwa mwaka wa fedha 2023/2024** kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ikihusu idhini ya kutekeleza ikama na bajeti kwa ajira mpya katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Maombi ya kujaza nafasi yoyote kati ya hizo yanakaribishwa kutoka kwa Mtanzania yoyote mwenye sifa zilizotajwa katika Tangazo hili:

### 1. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II - NAFASI TATU (3)

#### SIFA ZA MWOMBADI

Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliye hitimu mafunzo ya Stashahada au NTA Level 6 katika mojawapo ya fani ya Masijala kutoka katika vyuo vinavyotambuliwa na Serikali wenye ujuzi wa kompyuta.

#### MAJUKUMU YA KAZI.

- Kupanga na kudhibiti kumbukumbu/nyaraka katika vyumba vya kuhifadhi kumbukumbu (Repositories).
- Kushughulikia maombi ya kumbukumbu/nyaraka kutoka Wizara za Serikali na Taasisi zake.
- Kutafuta kumbukumbu/nyaraka zinazohitajiwa na wasomjaji.
- Kufanya ukarabati kumbukumbu zilizoharibika.
- Kuweka/kupanga kumbukumbu/nyaraka katika vyumba vya kuhifadhi nyaraka

#### MSAHARA

- Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya Serikali yaani **TGS.C** kwa mwezi.

#### NB: MASHARTI YA JUMLA:

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kati ya miaka 18 hadi 45.
2. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenyenye anuanini na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.

3. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, maelezo binafsi, vyeti vya Kidato cha nne au kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa husika na Picha moja "Passport Size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma. **Viambatanisho hivyo vibanwe sawa sawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea.**
4. Kwa waombaji waliosoma nje ya nchi elimu ya kidato cha nne na/au kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).
5. Kwa waliohitimu elimu ya chuo nje ya nchi, wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Elimu ya Ufundji la Taifa (NACTE).
6. **Testimonials "Provisional Results" Statement of results; hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
7. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
8. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi; wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria.
9. Waombaji wote watakaokidhi vigezo ndiyo watakaoitwa kwenye usaili (Interview)
10. Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoanishwa hayatashughulikiwa.
11. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **14 Agosti, 2024 saa 9:30 Alasiri**.
12. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na barua ya maombi isainiwe na kuambatishwa na vielelezo vinavyohitajika na yatumwe kuititia posta kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,  
Halmashauri ya Wilaya,  
S.L.P. 584,  
Korogwe.

Au

District Executive Director,  
Korogwe District Council,  
P.O. Box 584,  
Korogwe.

NB: Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe [www.korogwedc.go.tz](http://www.korogwedc.go.tz)

  
 David J. Mpumilwa  
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)

